

**KAULI YA WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO BUNGENI, DODOMA  
TAR.16/11/2018 KUHUSU MASHINDANO YA PILI YA RIADHA YA WANAWAKE NCHINI  
YATAKAYOFANYIKA DAR ES SALAAM TAREHE 24 NA 25/11/2018**

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa kushirikiana na Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Japan (JICA) itaendesha mashindano ya pili kwa wanawake kutoka mikoa yote nchini katika Uwanja wa Taifa Dar es Salaam tarehe 24&25 Novemba, 2018. Lengo la mashindano haya ya riadha ni kuibua vipaji katika riadha vilivyofichika upande wa wanawake, vipaji ambavyo Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa michezo, itavilea ili vifikie viwango vya kimataifa na kuweza kuiwakilisha nchi kwenye mashindano makubwa ya kimataifa yajayo k.m. Mashindano ya All Africa Games yatakayofanyika Casablanca, Morocco mwakani na Mashindano ya Olimpiki yatakayofanyika nchini Japan mwaka 2020.

Kama ilivyokuwa kwa mashindano haya mwaka jana, watoto wa kike wanaofanya vizuri wanapewa fursa kushiriki kwenye mashindano mbalimbali ya riadha ya kimataifa yakiwemo ya mbio ndefu ya Nagai, Japan yanayofanyika kila mwaka. Washindi wetu wa mwaka jana (wasichana 2 kutoka Arusha na 1 kutoka Mwanza (Ukerewe)) waliwakilisha nchi kwenye mashindano ya marathon ya Nagai, Japan mwezi Oktoba mwaka huu, na wote watatu walirejea na medali. Sylvia Masani kutoka Ukerewe, Mwanza, alipata medali ya shaba; Rozalia Fabian kutoka Arusha alipata medali ya fedha na Amina Mohamed vilevile kutoka Arusha alipata medali ya dhahabu.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kuwapongeza waheshimiwa Wakuu wa Mikoa ya Arusha na Mwanza na wakuu wao wa wilaya, na vilvile waheshimiwa Wabunge wote wa mikoa hiyo kwa malezi na maandalizi mazuri ya vijana wao hadi kuanza kufanikiwa kimataifa katika riadha. Nitumie fursa hii vilevile kuwahimiza waheshimiwa Wabunge wote kuhakikisha kuwa mikoa yao inashiriki kikamilifu kwenye mashindano ya riadha ya watoto wa kike tarehe 24&25 mwezi huu wa Novemba jijini Dar es Salaam. Mpaka sasa mikoa yote ya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar imetibitisha kushiriki isipokuwa mikoa minne ambayo leo sitaitaja kwa kuamini kuwa ndani ya siku chache itatibitisha.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.



Dkt. Harrison George Mwakyembe (Mb),  
**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO,**  
16/11/2018.





**KAULI YA WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO BUNGENI, DODOMA  
TAR.16/11/2018 KUHUSU MASHINDANO YA PILI YA RIADHA YA WANAWAKE NCHINI  
YATAKAYOFANYIKA DAR ES SALAAM TAREHE 24 NA 25/11/2018**

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa kushirikiana na Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Japan (JICA) itaendesha mashindano ya pili kwa wanawake kutoka mikoa yote nchini katika Uwanja wa Taifa Dar es Salaam tarehe 24&25 Novemba, 2018. Lengo la mashindano haya ya riadha ni kuibua vipaji katika riadha vilivyofichika upande wa wanawake, vipaji ambavyo Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa michezo, itavilea ili vifikie viwango vya kimataifa na kuweza kuiwakilisha nchi kwenye mashindano makubwa ya kimataifa yajayo k.m. Mashindano ya All Africa Games yatakayofanyika Casablanca, Morocco mwakani na Mashindano ya Olimpiki yatakayofanyika nchini Japan mwaka 2020.

Kama ilivyokuwa kwa mashindano haya mwaka jana, watoto wa kike wanaofanya vizuri wanapewa fursa kushiriki kwenye mashindano mbalimbali ya riadha ya kimataifa yakiwemo ya mbio ndefu ya Nagai, Japan yanayofanyika kila mwaka. Washindi wetu wa mwaka jana (wasichana 2 kutoka Arusha na 1 kutoka Mwanza (Ukerewe)) waliwakilisha nchi kwenye mashindano ya marathon ya Nagai, Japan mwezi Oktoba mwaka huu, na wote watatu walirejea na medali. Sylvia Masani kutoka Ukerewe, Mwanza, alipata medali ya shaba; Rozalia Fabian kutoka Arusha alipata medali ya fedha na Amina Mohamed vilevile kutoka Arusha alipata medali ya dhahabu.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kuwapongeza waheshimiwa Wakuu wa Mikoa ya Arusha na Mwanza na wakuu wao wa wilaya, na vilvile waheshimiwa Wabunge wote wa mikoa hiyo kwa malezi na maandalizi mazuri ya vijana wao hadi kuanza kufanikiwa kimataifa katika riadha. Nitumie fursa hii vilevile kuwahimiza waheshimiwa Wabunge wote kuhakikisha kuwa mikoa yao inashiriki kikamilifu kwenye mashindano ya riadha ya watoto wa kike tarehe 24&25 mwezi huu wa Novemba jijini Dar es Salaam. Mpaka sasa mikoa yote ya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar imetibitisha kushiriki isipokuwa mikoa minne ambayo leo sitaitaja kwa kuamini kuwa ndani ya siku chache itatibitisha.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.



Dkt. Harrison George Mwakyembe (Mb),  
**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO,**  
16/11/2018.

